

Learning by Ear 2009
 Children's rights and working for peace series
 Episode No. 08: Children's Prisons
 Author: Yaya Boudani (Burkina Faso)

Learning by Ear 2009 Children's Rights Series 08 Children's Prisons

Subject: Life in prison, how to prepare for rehabilitation?

Author: Yaya Boudani (Burkina Faso)

Editor: Sandrine Blanchard

Translator: Anne Thomas

Kisuaheli Eric Ponda

	Women	Men	Age	Language
IN/OUTRO		X	Unimportant	
Narrator	X		Ca. 25	
Luc Zina (Director)		X	Ca. 40	French
Jean-Martin Dabiré (social educator)		X	Ca. 40	French
Enriquet male prisoner 1		X	Ca. 15	French
Pablo male prisoner 2		X	Ca. 20	French
Franceline Female prisoner	X		Ca. 15	Mooré
Adama				French

Learning by Ear 2009
 Children's rights and working for peace series
 Episode No. 08: Children's Prisons
 Author: Yaya Boudani (Burkina Faso)

Traoré		X	Ca. 35	
Adeline Female prisoner	X		Ca. 30	French
Pierre Male prisoner (carpentry)		X	Ca. 25	French
Barthélémy (teacher)		X	Ca. 45	French
Pupil- prisoner male (moral)		X	Ca. 18	French
Edith (sewing)	X		Ca. 35	French
Old male prisoner		X	Ca. 55	Mooré

LbE Soundtrack

INTRO:

Hujambo mpenzi msikilizaji mahali popote ulipo na karibu kwa makala yetu ya 8 na ya mwisho kwenye mfululizo wa vipindi hivi vya “Noa Bongo Jenga Maisha Yako” kuhusu Haki za Watoto na juhudi zinazofanywa kudumisha Amani.

Safari yetu ya mwisho inatupeleka hadi nchini Burkina Faso, sio kutalii bali kuchunguza suala ambalo ni nadra sana kuzungumziwa, na ambalo hatujalifahamu vyema. Tunalitembelea gereza la MACO mjini Ouagadougou. Tutakutana na watu kadhaa - vijana kwa wazee ambao wamekuwa wakizuiliwa katika gereza hili kwa miaka mingi.

Report

1. Atmo: conversation 0'49

Narrator:

Gereza hili liko katikati mwa mji wa Ouagadougou. Lakini si wakaazi wengi wa jiji hili wanaofahamu kinachoendelea katika gereza hili

ambalo milango yake ya rangi ya samawati daima huwa imefungwa.
Ua wa seng'enge unaolizunguka gereza hili sio tu kuwazuia
wafungwa kutoroka bali pia wapita njia.

1. Atmo: conversation up

Narrator:

Askari mmoja wa magereza aliyejijami anafungua lango linaloelekea gerezani humo. Wageni wanaozuru gereza hili kawaida huandamana na wawakilishi kutoka wizara ya Huduma za jamii na mkurugenzi wa gereza hilo la MACO.

Gereza hili la MACO ndilo kubwa zaidi nchini humo na linakumbwa na matatizo mengi. Luc Yina ni mkurugenzi wa gereza hili.

2. sound luc overpopulation (French) 0'18

“Kuna uhaba wa vyumba vya kuwaweka wafungwa. Hili ni gereza kubwa linalowazuilia wafungwa wengi zaidi hapa nchini. Mwanzoni lilikusudiwa kuwahudumia wafungwa 500 lakini sasa kuna zaidi ya wafungwa 1349,— mara tatu zaidi ya idadi iliyokusudiwa. Tuna wafungwa 66 ambao ni watoto na nakiri hadharani kwamba tunakumbwa na tatizo kubwa la nafasi.”

Narrator:

Katika gereza hili hakuna mahali pa kulala au kumpumzika. Hata kwa watoto wadogo. Na gharama zinazidi kupanda. Ndio sababu serikali ina mipango ya kujenga vituo vingine vya kurekebisha tabia nchini humo. Tatizo jingine katika gereza hilo la MACO ni uhaba wa chakula. Hapa wafungwa hupewa chakula cha mchana pekee huku siku inayosalia wakibaki wakinywa maji na kumeza mate tu.

Jean-Martin Dabiré ni mkufunzi wa kijamii. Yeye hufanya kazi katika gereza moja mashariki mwa Burkina Faso, na anafhamu vyema kwamba kiasi cha faranga 150 sawa na senti 25 zinazotengewa kila mfungwa hakitoshi kugharamia chakula.

3. sound dabiré (French) 0'15

Lakini kutokana na ufadhili wa mashirika kadhaa kama vile shirika la wafungwa wasio na mipaka, tunajaribu kuhakikisha angalau supu kwa wafungwa hao. Lakini kusema kweli chakula hakitoshi. Hali ni ngumu kubwa hasa kwa wale ambao hawapati msaada wowote kutoka kwa wazazi wao.

Narrator:

Mbali na njaa, ni vigumu kwa wafungwa kukabiliana na kutengwa na kukaribiana Unaweza kusema ni **ukweli kinza** lakini sivyo kabisa. Wafungwa hawapati muda wa kutangamana na familia na marafiki zao walio nje lakini wamesongamana gerezamni na hawawezi kuwa na mahusiano ya kimapenzi. Luc Zina anasema kuwa hili si suala

linalosababishwa na idadi kubwa ya wafungwa, ni ukosefu wa mpangilio na uhaba wa rasilimali.

4. son luc separation 0'14

Hapa wafungwa wa kiume wametengwa kabisa na walr wa kike, na watoto pia wametenga na watu wazima. Hii ni kwa sababu uhaba wa vyumba vya kuwaweka wafungwa.

Narrator:

Katika magereza mengi humu nchini shirika la wafungwa wasio na mipaka limejenga vyumba vya watoto wafungwa, ili waweze kutengwa na watu wazima. Kila mfungwa anazuiliwa katika chumba cha ukubwa wa mita moja mraba.

5. Atmo congratulations 0'23

Narrator:

Ilituchukua muda wa miezi kadhaa kupata idhini kutoka kwa wizara ya sheria, lakini juhudi hizo zilikuwa za manufaa makubwa, kwani wafungwa walifurahi sana kutupokea kama wageni wao. Licha kwamba wanatoka matabaka mbalimbali, wote wanakumbwa na matatizo sawa- kuteswa na kunyimwa haki zao wakiwa gerezani.

Enriquet, mwenye umri wa miaka 15, alikuwa mfungwa wa kwanza tuliyemtembela gerezani humo. Yeye anatumika kifungo baada ya kupatikana na hatia ya kumuua kijana mwenzake waliozozana.

6. Enriquet (Français) 0'16

Mara nyingine huwa hatujui tulnalofanya. Kwani nisingelikuwa nimetenda kosa hilo. Lakini kwa kuwa tayari yamemwagika, nakiri makosa na kubeba jukumu hilo. Sikua namfahamu kijana huyo ila tu nilikutana naye asubuhi moja na akaanza kunitusi. Aliendelea kunitusi hata baada ya kumkanya-na hapo nikashikwa na hasira na kumpiga.

Narrator:

Pablo alikuwa fundi wa magari. Hakuwa akipata pesa nyingi kuishi maisha ya kifahari aliyotaka, na hivyo alijiingiza katika vitendo vya uhalifu.

7. Pablo (Français) 0'12

Nilipokuwa huko nje, nilitaka kuishi maisha ya kifahari, kutaka pesa na vitu vya bwerere na nikasahau maisha yangu ya baadaye. Hilo ndilo lililonitumbukiza gerezani.

Narrator:

Franceline ana hadithi tofauti.

8. Franceline 1 (Langue locale) 0'08

Nilikuwa nikiishi na Kakangu na Mkewe katika nyumba moja. Siku moja wakazozana. Shemeji yangu alitoroka na mimi nikamfuata.

Narrator:

Franceline anasema kuwa Kakake alimlazimisha kusema uongo. Alimshinikiza kusema uongo dhidi ya mkewe kwamba alinishawishi kumwekea sumu kakake.

9. Franceline 2 (Local language) 0'05

Nilisema alichokitaka na nikakamatwa wakati ule uleo mke wake alipokamatwa.

10. Atmo kitchen 1'46

Narrator:

Siku huwa ndefu sana hapa gerezani. Wafungwa hujaribu kujishughulisha kadri wawezavyo angalau kupoteza wakati. Jean-Martin Dabiré, mshauri wa kijamii anasema kuwa athari za kimwili na kisaikolojia zinazochangia hali ya msongamano na kutokuwa na kazi ya kufanya ni ngumu.

11. Dabiré : inactivity in prison (French) 0'25

Kimsingi hakuna kazi ya kufanya, hivyo wafunga huwa na dalili zinazohusiana na kukaa bila kazi. Miguu huanza kuvimba na mara nyingi wanapelekwa hospitalini kwa matibabu. Ukosefu wa mafunzo ya taaluma pia ni tatizo. Kwa kawaida wanakuwa hawana ajira kabla kwenda gerezani, na wakati wanapotoka wanakuwa hawajajifunza kitu chochote.

Narrator:

Kwa ushirikiano wa mashirika mbali mbali yasiyo ya kiserikali, gereza hili la MACO sasa limeanzisha miradi ya kuondoa upweke. Warsha zimeanza kuandaliwa ili kuwawezesha wafungwa kutangamana vyema na jamaa zao punde wanapotoka jela. Katika jela ya wanawake, kuna mafunzo ya upishi na ushonaji huku wengine wakijiunga katika mchezo wa kandanda. Adeline anasema anapendelea kazi ya mikono.

12. Adeline activités (Français) 0'12

Wengine hupika, na wengine kushona. Kuna shule ya kujifunza lugha ya taifa na kutengeneza sabuni. Mimi nashona.

!!! Maybe : KR 10_prison Atmo carpentry workshop !!! LbE/prod

Narrator:

Kazi ya kushona na useremala huwa san asana ni za wanaume.
Pierre anajifunza kazi ya uhomeleaji vyuma.

13. Pierre: workshop (French) 0'29

Mimi hutengeneza milango, madirisha ya vyuma na kadhalika. Mkufunzi wangu alinifunza mambo yote haya na nafurahia kazi hii sana. Nitakapotoka gerezani nitaweza kutengeneza milango na nadirisha ya vyuma. Kila kitu hutegemea uamuzi na bidii yako. Unapotoka gerezani inapaswa kuonekana mtu aliyebadilika na kutenda yaliyomema kwa bidii zako. Na kudhihirisha kuwa hapa gerezani tunapata ushauri, maafisa hutushauri jinsi ya kukabiliana na changamoto za maisha

14. Atmo reading 0'22

Narrator:

Pia kuna Barthélémy, mwalimu anayefundisha kusoma na kuandika lugha ya taifa.

15. Barthélemy : literacy (French) 0'12

Wafungwa hujifunza kusoma na kuandika kwa muda wa siku tano kwa wiki. Masomo yanaendelea vizuri na naweza kukuhakikishia kwamba ndio shughuli kubwa miongoni mwa Watoto wafungwa.

Narrator:

Si kazi rahisi kuanzisha darasa hapa gerezani, kwa sababu wanafunzi wengi wanatumika vifungo tofauti tofauti. Edith Ouedraogo, msimamizi wa miradi ya jamii katika gereza la MACO, anaeleza:

16. Edith : sewing workshop (Français)0'14

Mafunzo ya ushonaji yanaendelea vyema. Lakini shida moja ni kwamba kwamba mara nyingi hatujui mfungwa huyo atatumikia kifungo cha muda gani. Anaweza kuanza kujifunza kushona halafu baada ya muda mfupi anaondoka.

17. Atmo sewing workshop 0'38

Narrator:

Kwa ufupi juhudi zozote za kuwapa mafunzo na kuwarekebisha wafungwa ili waweze kuwa watu wa tabia njema katika jamii huwa ngumu sana. Mara nyingi wanapotoka gerezani hujikuta katika hali ile ile ya umaskini na kuandamwa na matatizo mengineyo. Na wakati mwengine hali hii huwa hatari zaidi kwa sababu wameishi na wahalifu gerezani na kisha ghafla kurudi katika mazingira hayo hayo. Adama Traoré anatoka shirika la wafungwa wasio na mipaka na anaeleza sababu zake.

18. Traoré: reasons for failure (French) 0'27

Ni ukosefu wa kazi ya kufanya kabla na hata baada ya kutoka gerezani. Wafungwa hawana kazi ya kufanya. Hawana kazi bali kupiga gumzo na kuelezana tabiazo mbaya. Ndio sababu mpango wa kuwatanganisha tena wafungwa wa zamani katika jamii umeshindwa kufanya kazi kwa wafungwa wengi. Shirika la wafungwa wasio na mipaka lina mipango ya kuanzisha vituo vya kuwasaidia waliokuwa wafungwa zamani ili kurejea katika maisha yao ya kawaida.

Narrator:

Kimsingi somo katika hadithi hii ni kwamba ni bora kujiepusha na vitendo vya uhalifu vinavyoweza kukuweka gerezani. Hiyo ndio kauli mbiu ya wafungwa wa gereza hili la MACO. Wadogo kwa wakubwa wake kwa waume, wote wanajutia vitendo vyao vilivyowapeleka gerezani.

19. Adeline advice (French) 0'09

Tunawashauri marafiki zetu wafikirie sana wanachofanya. Tayari sisi tuko hapa na hatungependa kuwashauri wao kuongeza idadi ya wafungwa hapa.

20. Pierre advice (French) 0'05

Wasithubutu kutamani pesa au vitu vya bwerere. Wizi si kazi.

21. advice old prisoner (local language) 0'17

Mimi nilihukumiwa kifungo cha miaka 20 gerezani. Nimepitia kila aina ya mateso. Na kweli nimefahamu kwamba mwanamume hupitia maisha magumu. Nawashauri vijana wazingatie taaluma zinazoweza kuwasaidia maihani. Gereza si mahali pazuri kabisa kunamharibia mtu maisha yake.

End music

OUTRO :

Na hadi hapo basi ndipo tunapofika mwisho wa kipindi. Ripoti hii imeatayarishwa na Yaya Boudani. Shukrani zetu kwa wafungwa na maafisa wa gereza la Ouagadougou kwa ushirikiano wao. Unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao; tovuti yetu ni: www.dw-world.de/lbe Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.!

End music